



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU

Unapojibu Tafadhali taja:

Tarehe 03/02/2022

Kumb. Na TDC/L.40/21/Vol III/62

### TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa na nia ya Kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kuomba nafasi (1) ya **Mtendaji wa Kijiji III** baada ya kupata kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb Na FA.170/367/01 'Temp'/62 cha tarehe 21 Desemba, 2021 kama ifuatavyo:

#### **MTENDAJI WA KIJIKI III NAFASI- MOJA (1)**

#### **SIFA:**

- Awe na Elimu ya Kidato cha IV au VI.
- Awe na Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii Kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### **KAZI NA MAJUKUMU**

- Afisa Masuuli na mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- Kuratibu na Kusimamia upangaji wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- Kutafsiri na kusimamia Sera, sheria na taratibu.
- Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalam katika Kijiji.
- Kusimamia Utungaji wa sheria ndogo za Kijiji.

- Kupokea, Kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.

### **Masharti ya Jumla**

- (a) Mwombaji awe Raia wa Tanzania ambaye ana umri si zaidi ya miaka 45.
- (b) Barua ya maombi iambatane na wasifu binafsi wa mwombaji wa hivi karibuni (Curriculum Vitae)
- (c) Barua ya maombi iambatanishwe na nakala ya vivuli vya vyeti vya Kidato cha IV, Kidato cha IV, Cheti cha Kuzaliwa, na vyeti vingine vya Taaluma.
- (d) Picha mbili ndogo (passport size) za hivi karibuni.
- (e) Matokeo ya Muda (Provisional/Testimonials/Statement of results) Hayatakubalika.
- (f) Watumishi ambao ni waajiriwa wa Serikali maombi yao lazima yapitishwe na waajiri wao.
- (g) Waombaji wenye Vyeti vya kidato cha nne na sita waliosoma nje ya nchi wanatakiwa kuwasilisha Uthibitisho wa NECTA.
- (h) Waombaji wenye vyeti vya Astashahada/cheti vya nje ya nchi wanatakiwa kuambatanisha uthibitisho wa NACTE.
- (i) Barua ya Maombi iandikwe kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.
- (j) Mwombaji wa ajira atalazimika kuwa na namba ya utambulisho wa Uraia (National Identification Number) kutoka mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)
- (k) Mwisho wa Kupokea maombi ni tarehe **16/02/2022 saa 9:30 Alasiri.**
- (l) Waombaji watakaokidhi sifa zinazotakiwa ndio pekee watakaoitwa katika Usaili.

**Barua zote zitumwe kwa njia ya posta kwa:**

**Mkurugenzi Mtendaji,**

**Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru**

**S L P 275**

**Tunduru.**

**Imetolewa na:**

Chiza C. Marando

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**TUNDURU**